# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,**
Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehma na mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuzidishie kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awazidishie busara pamoja na hekima katika kutekeleza jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Uongozi nzima wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawasisitiza wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia hatua ya malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**,
Kwa kweli, nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *9.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, Kanuni ya *108(15)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya utangulizi huo, sasa naomba kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambapo jumla ya mapendekezo 45 tuliyoyawasilisha kwa Wizara na yote tunashukuru yameweza kupatiwa majibu.

## WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI ZANZIBAR (ZGP)

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati inapenda kuchukua fursa hii adhimu kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza kwa vitendo uanzishaji wa Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisi na Kuandikia ambapo Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa kwenda kupata huduma za uchapishaji pamoja na vifaa vya ofisini kwa Wakala wa Uchapishaji wa Serikali Zanzibar (ZGP), lengo ni kupunguza na hatimae kuondosha kabisa matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,**
Pamoja na lengo hilo zuri la Serikali ya Mapinduzi ya Zanziba, lakini bado Wakala wa Uchapaji wa Serikali inakabiliwa na changamoto ya maghala kwa ajili ya kutoa huduma za Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisini na Kuandikia kwa Unguja na kupelekea kuendelea kukodi majengo kwa ajili ya uwekaji wa vifaa hivyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaona hali hiyo sio nzuri sana kwa sababu fedha nyingi za Serikali zinatumika kwa ajili ya kukodi jengo la kutolea huduma za Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisini na Kuandikia. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa ghala hata kama kwenye eneo la Wakala wa Uchapaji ama sehemu nyengine yoyote itakayofaa ili kuokoa fedha za Serikali zinazotumika katika kukodi jengo kwa bohari hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inapongeza juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuona upo umuhimu wa uwepo wa Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisini na Kuandikia kwa upande wa Pemba, ambapo hadi Kamati inawasilisha Hotuba hii Wakala wa Uchapaji tayari umeshapatiwa hati ya kiwanja kwa upande mmoja hili ni jambo jema, hivyo tunaomba Wizara kusimamia katika kufanikisha utekelezaji wake.

Kufanya hivyo, kutawezesha kufikia azma ya uanzishwa wa Bohari hii kwa Zanzibar na hatimae Taasisi zote za Serikali ziachane na mfumo wa ununuzi wa Vifaa vya Ofisini na Kuandikia kwa watu binafsi. Hivyo, kusaidia kuokoa fedha nyingi za Serikali ambazo

zilikuwa zikipotea kwa ajili ya manunuzi ya Vifaa vya Ofisi kinyume na utaratibu uliopo Kisheria.

## SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA ZANZIBAR (ZBC)

**Mheshimiwa Spika,**
Licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), bado Shirika linakabiliwa na changamoto ya uwepo wa Muundo wa Utumishi uliopitwa na wakati, hali ambayo inayopelekea kwa baadhi ya Wakuu wa Vituo kutokutambulika na kupelekea kukosa maslahi yao pamoja na stahiki zao nyengine kama Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 inavyoelekeza, kwani kutokuwepo kwa Muundo huo unakwenda na wakati kunapelekea kuwavunja morali wafanyakazi wa Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati kutokana na changamoto hiyo, inalishauri Shirika la Utangazaji la Zanzibar kuharakisha kuwasilisha Mapendekezo ya Muundo Mpya wa Shirika kwa Bodi ya Shirika kwa ajili ya kupata baraka na hatimae kuweza kuwasilishwa Tume ya Utumishi Serikalini. Kwa taarifa walizopatiwa Kamati kwamba Muundo unaotumika sasa ni ule uliopitishwa tangu mwaka 2016. Vile vile, Kamati inaishauri Wizara kupitia upya Sheria ya ZBC ya Nambari 4 ya Mwaka 2013, ili sheria hiyo ipate kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na ufanisi wa shirika.

## BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,**
Moja kati ya ushauri uliopendekezwa na Kamati katika Ripoti yake ya mwaka 2021/2022 iliitaka Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kukaa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kulitafutia ufumbuzi suala zima la urejeshwaji wa fedha walizokabidhiwa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa ajili ya kazi ya Mradi wa Ujenzi wa Green House 19 kwa Unguja na Pemba pamoja na uchimbaji wa visima katika mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, mpaka inawasilisha Hotuba hii bado ushauri wake haujafanyiwa kazi kuhusiana na urejeshaji wa fedha za uchimbaji wa visima kwa baadhi ya Green House zilizoshindikana kupatikana kwa huduma ya maji. Hivyo, Kamati inaendelea kuiomba Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kurejesha fedha hizo, ili ziweze kutumika katika kuimarisha miradi iliyoanzishwa kupitia Baraza la Vijana ambayo bado inakumbwa na changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji.

## SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa Shirika la Magazeti, miongoni mwa sababu kuu ambazo zinazopelekea Shirika kutokuweza kujiendesha kwa asilimia mia moja ni uwepo wa madeni makubwa na ya muda mrefu yanayopelekea kudhorotesha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, ambapo kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi tunawasilisha hotuba hii wanadaiwa shilingi Bilioni Mbili, Milioni Tisiini na Sita, Laki Nne, Hamsini na na Sita na Mia Mbili na Mbili (2,096,456,202/=) na kwa upande wa Tanzania Bara ni shilingi Milioni Mia Nne na Sabiini na Mbili, Laki Saba na Hamsini na Tatu na Mia Mbili (472,753,200/=). Jumla ya deni hilo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano na Sitini na Tisa, Laki Mbili na Tisa, Mia Nne na Mbili (2,569,209,402/=) hadi tarehe 30 Juni, 2022.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho, Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya maelezo hayo machache, naomba kuwasilisha.

Ahsante,


……………………,
Mhe. Mohamed Ahmada Salum,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**